Taarifa kwa Vyombo vya Habari
Kwa utangazaji wa haraka

# Vijana wenye kipaji cha zana za teknolojia waweka takwimu za elimu wazi

Mkutano wa Ushirika wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi (OGP) ukiwa unaadhimishwa, wavuti mpya unaokusanya na kuonyesha takwimu za matokeo ya Kidato cha 4 zikiwa zimenyumbuliwa, umezinduliwa.

**Dar es Salaam, 31 Oktoba 2013:** Mkutano wa Ushirika wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi (OGP) umezinduliwa rasmi jijini London, Uingereza, na mwaliko wa kuhudhiria katika mkutano huu umemfikia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Jakaya Kikwete. Umoja wa vijana nchini wakitumia fursa ya mkutano huu, wakiwa wataalamu wa zana za teknolojia, wamezindua wavuti uitwao *shule.info* ili kuonyesha umuhimu wa takwimu zilizo wazi. Wavuti hii unakusanya takwimu za matokeo ya mitihani ya Kidato cha 4 kuanzia mwaka 2004 na kuzipanga katika namna ambayo ina urahisi wa kusoma na wepesi wa kueleweka.

Arnold Minde na timu yake, wakitumia nafasi zao za pekee, walitumia muda wa takribani miaka miwili, kukusanya takwimu za matokeo ya kidato cha 4 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo mitandao tofauti tofauti. Kwa kuwa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) halikuzifanya takwimu hizi kupatikana kwa urahisi na kwa wakati katika tovuti yake, timu hii ililazimika kutumia muda mwingi sana kuzitafuta na kuzikusanya.

Inatarajiwa kuwa wavuti hii itakuwa wa muhimu sana kwa wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo wazazi na watunga sera, ambao wote kwa pamoja wataweza kupata takwimu wanazozihitaji kwa urahisi. Watunga sera wataweza kuzitumia takwimu za shule moja moja na mikoa na kutazama wapi kumekuwa na mafanikio na wapi pameanguka, wakati wazazi wataweza kulinganisha shule na kufanya uamuzi kutokana na taarifa hizo kuwa wawapeleke watoto wao katika shule zipi. Wanafunzi nao watafanikiwa kupata kadi zao za matokeo kwa kuingiza namba zao za utahiniwa na vituo vya mitihani. Majina ya watahiniwa hayajawekwa katika tovuti hii bali mwanafunzi atatambulika kwa namba yake ya utahiniwa.

Wavuti hii pia umeundwa ili kuwa chanzo cha taarifa kwa vyombo vya habari na kuripoti kuhusu mienendo ya matokeo, kuonyesha maeneo yanayong'aa na kuchunguza masuala yanayoonekana kutoenda sawa. Wavuti hii unatoa fursa ya hatua nyngi kuchukuliwa iwapo takwimu za matokeo zimewekwa wazi.

Katika muktadha wa Tanzania kujiunga na Ushihirika wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi, wavuti hii unatoa kielelezo bayana cha manufaa ya takwimu zilizo wazi. Pale raia wanaporuhusiwa kushiriki moja kwa moja katika shughuli za Serikali, kupitia upatikanaji wa takwimu na taarifa, uwezekano wa kuingiza ubunifu unakuwa ni mwingi. Nchi yetu imepiga hatua kwa kuingia katika awamu nyingine ya Serikali inayoendeshwa kwa wazi. Wavuti hii inaonyesha mfano wa ushirika mpya wa namna ya kuendesha Serikali, jambo ambalo ni kiini cha ushirika huu.

*"Takwimu zinazowekwa wazi siyo dhana tu inayoelea hewani katika makongamano ya viongozi wa juu,"* alisema Arnold Minde ambaye alishughulika sana katika kuitengeneza wavuti hii, *"Takwimu zilizo wazi ni hasa kuwezesha upatikanaji wa taarifa zinazozihitajika ili kuhakikisha kuwa Serikali inatimiza ahadi zake na kuwapa wananchi nafasi ya kuchangia mawazo na kutafuta suluhu kwa changamoto zinazolikabili taifa. Panapokuwa na takwimu zilizo wazi, kweli tunaweza kuungana na Serikali na wadau wengine katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu."*

Uhifadhi na upanuzi wa wavuti hiyo unafadhiliwa na shirika huru la Twaweza. RakeshRajani, Mkuu wa Twaweza na Mwenyekiti Mweza wa Vyama vya Kiraia katika Ushihirika wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi, anasema *“Inatia faraja sana kuona mioyo wa vijana hawa waliotengeneza wavuti hii ya Shule.info ikiwa inalenga maendeleo ya nchi yao, na vyote vilivyoingizwa katika wavuti hii vikiwa vya manufaa kwa Wananchi. Tumechagua kuonyesha kazi hii kwa madhumini ya kuonyesha mfano wa namna ambayo takwimu zinazowekwa wazi zinaweza kuwa za manufaa kwa nchi. Ni matumaini yetu kuwa wavuti hii itasaidia kuleta uwazi zaidi kwa upande wa Serikali katika kutoa takwimu kwa kuzingatia viwango vya takwimu zilizo wazi, na kuleta ushirikiano zaidi kati ya Serikali na makundi yanayojitegemea ili kufanya takwimu hizi zipatikane kwa watu walio wengi zaidi.”*

**---Ends---**

**Maelezo kwa Wahariri**

- Wavuti inapatikana kupitia www.shule.info
- Shule.info ni wavuti iliyo hai ambapo kwa sasa inapatikana kupitia program ya majaribio ya Beta. Maoni kuhusu wavuti hii yanakaribishwa kutoka kwa watu wote, hasa wanahabari kupitia anwani hii matokeo.shuleni@gmail.com
- Wavuti umeandaliwa na Arnold Minde na timu ya waendelezaji zana za teknolojia Watanzania, wakifadhiliwa na Twaweza. www.twaweza.org
- Tafadhali zingatia kwamba NECTA nayo pia hivi karibuni imezindua wavuti ya takwimu za mitihani inayopatikana kupitia anwani hii http://www.necta.go.tz/opentakwimu/
- OGP ilizinduliwa mwaka 2011 ili kuanzisha jukwaa la kimataifa kwa ajili ya waleta mabadiliko wa ndani ya nchi waliokuwa wanataka Serikali zao kuwa wazi zaidi, zinazowajibika zaidi na zinazowasikiliza wananchi wao. Tangu wakati huo, OGP imekua kutoka nchi 8 hadi 60 zinazoshiriki kama inavyoonyeshwa kwenye ramani hapa chini. Katika nchi zote hizi, Serikali na vyama vya kiraia vinashirikiana kuendeleza na kutekeleza mageuzi haya motomoto ya kuleta Serikali wazi. Soma zaidi katika anwani hii www.opengovpartnership.org
- Zaidi ya wajumbe 1,000 kutoka katika nchi 60 watakutana jijini London kuanzia tarehe 31 Oktoba hadi 1 Novemba kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Ushirika wa Serikali Wazi. www.gov.uk/government/topical-events/open-government-partnership-summit-2013